JAMHURI YA YA MUUNGANO YA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA WATOA HUDUMA ZA MAUDHUI KWA NJIA YA MTANDAO

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kukiri mwitikio mzuri wa wamiliki wa Blogu, Majukwaa mtandaoni (online forums), Radio na Televisheni za mtandaoni wanaoendelea kujitokeza katika zoezi la usajili tokea tulipotoa tangazo tarehe 21 Aprili, 2018.

Aidha, TCRA inapenda kutoa ufafanuzi juu ya maswali mbali mbali ambayo yamekuwa yakiulizwa kama ifuatavyo:-

| Na. | SWALI | UFAFANUZI |
|---|---|---|
| 1. | Je, usajili huu unahusu pia Magrupu yanayotumia majukwaa/mitandao ya nje kama WhatsApp, Facebook, Instagram, n.k? | Usajili huu hauhusu watumiaji wa mitandao ya kijamii yenye wamiliki walioko nje ya nchi kama WhatsApp, Facebook, Instagram, n.k,<br><br>Hata hivyo, Kanuni ya **5, 7, 8** na **10** za Kanuni za Maudhui Mtandaoni (Online Content Regulations) za 2018, inawapa wajibu wa kutimiza watumiaji wote wa maudhui mitandaoni ikijumuisha wana-Group wote na Wasimamizi (Administrators) wake bila kujali unatumia majukwaa/mitandao ya ndani au ya nje. |
| 2. | Je, wamiliki wa ***websites*** nao wanatakiwa kujisajili? | Hapana iwapo haijihusishi na upakiaji wa taarifa za mara kwa mara (Current Affairs and News) vinginevyo itahitaji leseni kupitia usajili. |
| 3. | Je, wamiliki wa Radio na Televisheni walio na Leseni za TCRA kwa sasa lakini wanarusha pia matangazo yao kwa kutumia internet wanatakiwa kusajiliwa? | **Ndiyo**, Kwa wamiliki wa Radio na Televisheni ambao tayari wana leseni moja ya kurusha maudhui kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini na Maudhui yaleyale yatarushwa mtandaoni (simulcasting), wamiliki wake watatakiwa kuwa na leseni nyingine ya online redio/television. |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Je, usajili unafanyika kwenye mtandao pekee? | **Ndiyo**, fungua tovuti (website) ya TCRA (www.tcra.go.tz), upande wako wa kulia juu kuna maandishi yanasomeka (**BROADCASTING**) chini ya maandishi haya utaona linki yenye neno Online Content Application System bofya na uendelee na usajili. |
| 5. | Je, gharama za usajili ni kiasi gani? | Gharama za usajili ni kama zilivyofafanuliwa kwenye ***Jedwali AA*** hapa chini: |
| 6. | Muda wa Leseni ukoje? | Leseni zote ni za miaka mitatu ambapo baada ya muda huo itahitajika kuomba kuhuishwa na kupewa Leseni nyingine kwa anayekidhi vigezo husika. |

***Jedwali AA***

| ***SN*** | ***Aina ya Leseni*** | ***Gharama za Maombi ya usajili (Application Fee)*** | ***Ada ya kupatiwa Leseni (Initial Licence Fee)*** | ****Ada ya Mwaka ya Leseni (Annual Fee)*** | ***Gharama ya Kuhuhisha (renew) Leseni*** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ***Blogu, Majukwaa mtandaoni (online forums), na waombaji wapya wa Redio na Televisheni mtandaoni wasio na leseni ya Utangazaji unaotumia mitambo iliyosimikwa ardhini.(Terrestrial broadcasting services)*** | **TZS. 100,000.00** | **TZS. 1,000,000.00** | **TZS. 1,000,000.00** | **TZS. 1,000,000.00** |
| 2 | ***Televisheni mtandaoni (simulcasting)*** | **TZS. 50,000.00** | **TZS. 200,000.00** | **TZS. 200,000.00** | **TZS. 200,000.00** |
| 3 | ***Radio mtandaoni(simulcasting)*** | **TZS. 50,000.00** | **TZS. 200,000.00** | **TZS. 200,000.00** | **TZS. 200,000.00** |

Ada ya mwaka italipwa baada ya leseni kufikisha miezi 12 tangu itolewe.

Kwa ufafanuzi au maelezo zaidi tumia barua pepe: onlinecontent@tcra.go.tz
au Piga namba +255 22 2199769 au +255 22 2412011 wakati wa kazi.

IMETOLEWA NA:
MKURUGENZI MKUU
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
23 APRILI, 2018